JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0767 884095**

**0623 185 893**

**Makamu Mkuu wa Shule 0613 228 775**

**Shule ya Sekondari KIWELE**

**S.L.P 733**

**Tarehe ....................**

**Kumb.Na. KWSS/AD F V/VOL.1/07**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIWELE HALMASHAURI YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA .....................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ............. na atasoma tahasusi ya HGK, HGL, HKL, EGM, HGE, HGFa na HGLi ( kata isiyokuhusu).

Shule ya Sekondari KIWELE ipo umbali wa Kilometa 25 Magharibi mwa Mji wa Iringa Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi ya mjini / mfyome Nauli ni Shilingi 2000/= au kwa pikipiki na Shilingi 10,000/= au kwa bajaji shilingi 4000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ..............., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................ Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1Sare za Shule

i.Sare ya shule hii ni sketi mbili (02) rangi NYEUSI kitambaa KIZITO (ESTEM NAMBA MOJA). Zishonwe linda box kubwa mbele na nyuma na malinda madogo pembeni. Sketi iwe ndefu mpaka kwenye kisigino

ii.Mashati mawili (02) rangi nyeupe yasiyo na urembo wowote yenye mikono mirefu.

iii.Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama .

iv.Sare ya Michezo ni track suti ya DARKBLUE na tshirt ya rangi ya DAMU YA MZEE(MAROON) isiyo na maandishi.

v.Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi.Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Sweta mbili (02) rangi ya DARK BLUE yenye shingo ya ”v”.

iv.Nguo za kushindia (*shamba dress*) mbili (02) kitambaa Kizito rangi ya DARKBLUE (ESTEM NAMBA MOJA) ishonwe linda sita (yaani linda kubwa mbele na nyuma pembeni malinda madogo wawili kila upande) juu mikono kifupi ya kawaida. **Gauni liwe refu mpaka kwenye kisigino cha mguu.**

### 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa (counterbooks) 4quire kumi (10)

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi ( A ONE YENYE KAVA NYEKUNDU) Mbili (2) kwa mwaka. Zingatia aina ya ream uliyoandikiwa)

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwe*);

iv. Scientific Calculator kwa HGE, EGM, HGK na HGL

v. Godoro la 2½ × 6.

vi. Mashuka Jozi 2, ( lightblue 01 na pink 01) blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

- Chupi 6
- Tite 06
- Underskirt 3
- Singland 3

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) Yenye mifuniko.

x. Ni lazima mwanafunzi akaja na kadi ya **BIMA YA AFYA** au aje na tsh. **50,400/=** kwa ajili ya bima ya afya kwa matibabu ya mwaka mzima (NHIF). Kadi ya bima afya itakaguliwa au pesa itapokelewa siku ya kuripoti.

xi. Ni vema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni awe amechukua **tahadhari zote za kiafya.**

xii. Tochi 01

**2.5: Uhuru wa Kuabudu.**

Utaruhusiwa kuabudu kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi.

**2:7: Kubadili Dini.**

Hutaruhusiwa kubadili dini, ukiwa shuleni wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**2.8: Kubadili jina.**

Hautaruhusiwa kubadili jina. Jina lako linatakiwa kuwa kama ilivyotumika wakati wa mitihani wa kidato cha nne kwenye **SELF – FORM** yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili kutoka kipengele hiki, mwanafunzi anaporipoti shuleni, anatakiwa kuja na nakala (**Photocopy**) ya cheti chake cha kuzaliwa na Result slip. Hii itasaidia kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa usajili wa mtihani wa taifa.

**2.10: Mpango wa Usafiri.**

Mpango wa Usafiri. Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli. Usafiri wakufika Iringa ni kwa njia ya mabasi. Mwalimu wa usafiri atakusaidia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema, ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni. Katika hili tunaomba sana wazazi tusaidiane kulisimamia.

**2.11: Vitu visivyoruhusiwa shuleni.**

a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendana na simu) Mawasiliano muhimu baina ya mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafanyike kupitia kwa Mkuu wa Shule kwa anuani tajwa hapo juu.
b) Pasi za umeme, pasi ya mkaa, heater, birika la umeme
c) Kusuka nywele au kuweka dawa za aina yoyote ile
d) Kupaka rangi kucha au kupaka ina, wanja na lipstic
e) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule.
f) Heleni, Mkufu, pete na bangili

**2.12 VIFAA VINGINE;**

**HKL** Spedi ya chuma 01, mswaki wa kusafishia sink 01, kwanja 01 na chelewa 01

**HGK** Sepetu ya chuma 01(spedi ya chuma), kwanja 01, fagio ngumu (hardbloom 01) na fagio ya chelewa 01.

**HGE** Ndoo ya kudekia na fagio yake, kwanja 01 na fagio ya chelewa 01.

**EGM** Ndoo ya kudekia na fagio yake, kwanja 01 na fagio ya chelewa 01.
**HGL** Reki, mswaki wa kusafishia sink 01, kwanja 01, fagio ya chelewa.

**HGFa:** shoka yenye mpini lilonolewa 01, kwanja 01, hardbloom 01 na fagio ya chelewa 01,
**HGLi:** shoka yenye mpini lilonolewa 01, reki 01 na fagio ya chelewa

## 2.2 Michango mbalimbali

a) **Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: FEDHA ZOTE ZA MICHANGO ZILIPWE KWENYE AKAUNTI NAMBA 60501100071 MNB KIWERE SEKONDARI MWANAFUNZI AJE NA SLIPI TU NA SIO PESA**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye incha kali au dawa.

**Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba wa mzazi/mlezi au Ugonjwa)**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule ELIZABETH JOSEPH MALIGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0623 185 893**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0613 22877**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
SHULE YA SEKONDARI KIWELE

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO**

**SEHEMU YA KWANZA**
(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

| Picha |
|---|

1. Mimi ------------------------------------------------ (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Kwanza/Tano katika sekondari ya Kiwele.

   Jina la Mwanafunzi ----------------------------------------------------
   Sahihi ya mwanafunzi------------------------
   Tarehe ----/------/20---
2. Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi

   Mimi ----------------------------------------------------- Mzazi/Mlezi wa ------------------------
   Nakubali/Sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Viongozi na Jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

   Jina la Mzazi/ Mlezi --------------------------------------------------------

   Sahihi ----------------------------
   Tarehe ----/----/20-----

   Namba ya simu……………………………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**KIWELE SEKONDARI**

**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULE**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

**(Fomu hii ijazwe na mzazi/ mlezi iambatanishwe picha NNE ZA mzazi /mlezi atayekuwa anawasiliana na walimu shuleni au kumtembelea mwanafunzi**)

1. Jina kamili la baba ……………………………………………
2. Uraia ………………………
3. Kazi yake ……………………………………………….
4. Namba ya simu……………………………………
5. Jina kamili la mama …………………………………….
6. Uraia ……………………….
7. Kazi yake ………………………………………………………
8. Namba ya simu…………………………………………….
9. Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake)……………………………………………………………
10. Namba ya simu ……………………………………
11. Mtoto anaishi na (1) Baba tu (2) Mama tu (3) Wazazi wote (4) mlezi (kata yasiyohusika).
12. Dini ya mzazi/mlezi ……………………………………………………
13. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe …………………………….
14. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo…………………………………………………………
15. Mimi……………………………………………. Mzazi/mlezi wa ………………………………………. nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri mchapa kazi, na mwenye bidii.

…………………………..  ……………………………

Sahihi ya mzazi/mlezi.  Tarehe

**KIWELE SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**(To be completed by medical officer in suspect of all new students)**

Full name ……………………………………………………………….

Age …………………….

1. Blood count (red and white) ……………………………………….
2. Urine examination ……………………………………………… ….
3. Stool examination …………………………………………………...
4. Syphilis test ………………………………………………………….
5. T.B test ………………………………………………………………
6. Ear test ……………………………………………………………….
7. Eye test ……………………………………………………………….
8. Spleen ………………………………………………………………...
9. Abdomen …………………………………………………………….
10. Addition information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases.

    ………………………………………………………………………………

    ………………………………………………………………………………

    Treatment after examination.

    ………………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE**.

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ……………………………Designation …………………………….

Station ………………………………….

(Official Stamp) ……………………….

Date …………………………………….

**NB**: Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika Serikalini.

## ORODHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO SOMO LA ENGLISH LANGUAGE, LITERATURE IN ENGLISH , KISWAHILI NA FASIHI YA KISWAHILI

### ENGLISH LANGUAGE (HGL &HKL)

**NOVELS**

ANIMAL FARM – George Orwell
CHASING THE LEOPARD FINDING THE LION -Juliet Wakeman Linn
OPPOTUNIST – Nyambari. C.M. Nyangwine
THE HORIZON UNVELLED – Followers Mwaisela

**PLAYS**

A TASTE OF HEAVEN OF HEAVEN – Farouk Topan
THE GOVERNMENT INSPECTOR – Nikola V. Gogol

POETRY

LAMENT OF THE SILENT AND OTHER POEMS – Jared Angira

### LITERATURE IN ENGLISH (HGLi)

**NOVELS**

ALLOW OF GODSS – Chinua Achebe
A GRAIN OF WHEAT – Ngugi Wa Thiongo
PETAL OF BLOOD – Ngugi Wa Thiongo
NO LONGER AT EASE – Chinua Achebe

**PLAYS**

BETRAYAL IN THE CITY – Francs Imbuga
I WILL MARRY WHEN I WANT – Ngugi wa thiong'o & Ngugi wa Mirii
MAN OF KAFIRA - Francs Imbuga
JULIUS CAESAR – Willium Shakespare

**POETRY**

POETS OF AFRICA (BOUNDLESS VOICES, POEM OF KENYA) – Arthur Luvai
THE BLEEDING HEART AND OTHER POEMS – Shjilia Kaaya

### FASIHI YA KISWAHILI (HGFa)

**USHAHIRI**

DHIFA (2023) Euphrase Kezilohabi
UTENZI WA MAJUMUIWA KARNE YA 21 (2023) – Idd Mwimbe
MALENGA WA BARA (2023) – M.M. Mlokozi

**TAMTHILIYA**

KAPTULA LA MARX (2023) – Euphrase Kezilahabi
NYERERE NA SAFARI YA KANANI (2023) – Emmanuel Mbogo

**RIWAYA**

ASALI CHUNGU – Sais Ahmed Mohamed
MWANA WA YUNGI HULEWA (2023) – Mohamed Said Abdulla

**KISWAHILI II (HGK&HKL)**

**TAMTHILIYA**

MKWAVA WA UHEHE (2023) – M.M.Mlokozi
SHUJAA MILAMBO (2023) – Emmanuel Mbogo
USALITI MJINI (2024) - Fransis Imbuga

**USHAIRI**

FUMBO LA LINALOELEA (2023) – Nyambari C.M Nyangwine
MALENGA WA ZIWA KUU (2024) – Wallah Bin Wallah
ANDAMO MSAFIRI (2023) – Mohamed Khelef Ghassani
WOSIA WA BABA (2024) Ahmed Mohamed Amanzi

**RIWAYA**

DUNIA UWANJA WA FUJO (2023) Euphrase Kezilohabi
UA LA FARAJA (2007) – W.E.Mkufya
MIRATHI YA HATARI (2023) – C.G. Mungongo
WASIFU WA SITI BINTI SAADI (2023) – Shabani Robert

**Mkuu wa Shule 0767 884095**

**0623 185 893**

**Makamu Mkuu wa Shule 0613 228 775**